**Mradi wa Panda miti kibiashara utakavyobadilisha maisha ya wakazi wa Nyasa**

**Na Albano Midelo**

Mradi wa Panda miti kibiashara unaofadhiliwa na nchi ya Finland sasa umepiga hodi katika Mkoa wa Ruvuma.



Katika mkoa wa Ruvuma mradi huo uliofadhiliwa na nchi ya Finland unafanyika katika Halmashauri za Wilaya ya Nyasa,Mbinga na Madaba wilayani Songea.

Mshauri wa Misitu katika Mradi wa Panda Miti Kibiashara Sangito Sumari anasema katika wilaya ya Nyasa mradi huu unahusu miti

aina ya mitiki ambayo utafiti umebaini inastawi vizuri katika hali ya hewa iliyopo mwambao mwa ziwa Nyasa.

“Miche ya miti ya mitiki zaidi ya milioni moja iliyopo katika eneo la hekari 6.2 tayari imepandwa katika bustani ya Lipingo na inatarajiwa kupandwa katika hekta 700 zilizopo kando kando mwa milima ya Livingstone mwambao mwa ziwa Nyasa”,anasisitiza Sumari.

Anasema wakazi wa mwambao mwa ziwa Nyasa wataanza kunufaika kwa kuanza kuvuna katika kipindi cha miaka 15 ijayo na kwamba kila mwaka wanatarajia kupanda miche ya mitiki katika eneo lenye ukubwa wa hekta zaidi ya 700.

Sumari anabainisha kuwa mradi wa panda miti kibiashara unafanyika katika mikoa minne hapa nchini ukiwemo mkoa wa Morogoro mradi unatekelezwa katika wilaya mbili za Ulanga na Kilombero.

Mikoa mingine ni  Iringa mradi unatekelezwa katika wilaya za Kilolo na Mufindi,Mkoa wa Njombe mradi unafanyika wilaya ya Njombe,Makete na Ludewa na  mkoa wa Ruvuma katika wilaya za Nyasa,Songea na Mbinga.

Kwa mujibu wa Sumari mradi wa panda miti kibiashara ni wa miaka minne ulianza mwaka 2014 na  ulitarajiwa kukamilika Desemba 2017.Hata hivyo Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na wafadhili nchi ya Finland wameridhia mradi huu uongezewe mwaka mmoja kutokana na matokeo mazuri ya utekelezaji.

Bustani ya miche ya mitiki Lipingo inaendeshwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ambao wana ofisi ya Kanda mkoani Iringa,ambao wanazalisha miche ya mitiki katika Mradi wa Panda miti kibiashara.

“Miche hiyo itapandwa katika vijiji saba mwambao mwa ziwa Nyasa na baada ya miaka saba,meta moja ya ujazo ya magogo ya mitiki inaweza kutoa kati ya shilingi laki tano hadi laki nane,kwa wastani mtu akiwa na hekari moja anaweza kupata zaidi ya shilingi milioni 120”,anasisitiza Sumari.

Anasema miti hiyo ikianza kuvunwa itabadilisha maisha ya wakazi wa mwambao mwa ziwa Nyasa kwa kuwa viwanda ambavyo vitatumia malighafi ya mbao za mitiki vitaanzishwa na vijana watapata ajira.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Misitu na Nyuki wa Wizara ya Maliasili na Utalii Deusdedit Bwoyo anasema mradi wa panda miti kibiashara, ukihusisha miti aina ya mitiki utaleta maendeleo makubwa kutokana na thamani kubwa ya miti hiyo katika soko la ndani na nje ya nchi.

“Tunawaasa wananchi wa Nyasa kuchangamkia fursa ya kuotesha miti hii,serikali imetoa mbegu hizi kwa wananchi kwa faida yao,serikali itawapatia elimu ya kuendeleza miti hii ambayo itachangia kuondoa umaskini watakapoanza kuivuna na kuuza”,anasema Bwoyo.

Mshauri wa Balozi wa Finland nchini Tanzania Kari Leppanen anasema ana matarajio makubwa ya mradi huo kuwaondoa katika umaskini wakazi wa wilaya ya Nyasa.

Leppanen anabainisha kuwa mradi huu utatoa faida kubwa kwa wakulima wadogo ambao watazalisha miti hiyo ambayo itaanza kuwarudishia fedha zao kati ya miaka saba hadi 15 na kwamba wakulima wadogo wa mitiki watashiriki katika kuchangia Pato la Taifa.

Afisa Maliasili na Utalii wa wilaya ya Nyasa Bugingo Bugingo anasema mradi huo utahusisha vijiji saba katika eneo la kilometa 15, anavitaja vijiji vitakavyonufaika na mradi huo kuwa ni Lundo,Lipingo,Nkali A,Liuli, Nkalachi, Mango na Puulu.

Utafiti umebaini kuwa mitiki ni miti ambayo ina thamani kubwa ndani na nje ya nchi, miti hiyo inayostawi na kumea vizuri katika ukanda wa kitropiki na inahitaji mvua kwanzia mililita1000.

Ben Mfungo ni Rais wa Shirikisho la Viwanda vya Misitu Tanzania(SHIVIMITA) tangu mwaka 1988,anabainisha mahitaji ya soko la miti aina ya mitiki ni kubwa ndani na nje ya nchi.

"Juzi tu nilikuwa Accra nchini Ghana ,tulijulishwa kwamba Jumuiya ya ECOWAS ilichukua mbegu za miti ya mitiki toka Tanzania baada ya kubainika mbegu za Tanzania zina ubora zaidi katika soko la dunia hivyo nao wameamua kuchukua mbegu hiyo inayokidhi soko la kimataifa",anasisitiza Mfungo.

Anawaasa wakulima wapya wa mitiki katika wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma na maeneo mengine yakiwemo Mtibwa mkoani Morogoro,Muheza mkoani Tanga na maeneo mengine ambayo zao hilo linaweza kustawi, waongeze uzalishaji wa zao la mitiki kwa sababu tangu enzi hizo hadi leo mahitaji yake yanaendelea kuongezeka.

Anayataja miongoni mwa matumizi ya zao la mitiki kuwa ni kutengenezea vitako vya silaha aina ya bunduki,vyombo vya majini kama vile meli na boti,ujenzi wa mahakama kubwa duniani imetumika miti aina ya mitiki kwa sababu ndiyo mti mgumu ambao unaweza kuishi majini na nchi kavu,pia hutumika kutengeneza samani mbalimbali zenye gharama kubwa.

"Mahitaji ya mti huu katika soko la duniani ni makubwa ,ndiyo maana nchi za Ulaya na nchi za Asia zikiongozwa na China na India wananunua miti aina ya mitiki kwa wingi kutoka Tanzania,na hata hatujaweza kufikisha hata robo ya mahitaji yao",anasisitiza Mfungo.

Kutokana na hali hiyo Rais huyo wa SHIVIMITA anawatoa wasiwasi wakulima wa mitiki hapa Tanzania wasiwe na hofu ya soko la hapa nchini na nje ya nchi ambapo meta moja ya ujazo wa mitiki inauzwa zaidi ya dola 1000 ni zaidi ya shilingi milioni mbili.

Anasema miti hiyo tangu kupandwa hadi kuvunwa inachukua takriban miaka 15 na kwamba katika kipindi hicho watu wa mwambao mwa ziwa Nyasa watakuwa wanazungumzia Tanzania yenye viwanda kwa sababu miti hiyo itatumika kama malighafi za viwanda vitakavyojengwa mwambao mwa ziwa Nyasa kwa ajili ya kutengenezea boti na hata meli.

Anaitaja nchi ya Malyasia ambayo imepata mafanikio makubwa baada ya kuanzisha kilimo cha miti ya mitiki ambayo inasababisha nchi hiyo kupata mapato ya dola zaidi ya bilioni 13.

Ukiacha mradi wa miti aina ya mitiki ziwa Nyasa,mradi wa Panda miti kibiashara pia umeanzishwa katika Halmashauri ya mji wa Mbinga,Mradi umeweza kuzalisha miche bora ya miti milioni 1.2 katika kitalu cha miti Kihaha ambayo wamegawiwa wananchi bure na kuipanda ili waweze kuondokana na umaskini.

Miche hiyo imepandwa katika hekta 500 katika eneo la Lihumbe na Ukimo kata ya Mbangamao eneo la Lipilipili kata ya Mpepai.

Lengo kuu la mradi huo ambao unafadhiliwa na nchi ya Finland ni kuwasaidia wananchi maskini ambao wamejiunga kwenye vikundi katika maeneo hayo, ili waweze kuinua kipato chao kwa njia ya panda miti kibiashara.

Afisa Misitu wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga,David Hyera anasema kuwa miche ya miti iliyozalishwa kwenye kitalu hicho ni aina ya Milingoti (Eucalyptus) na Mikaratasi (Pines).

Hyera anabainisha kuwa miche aina ya Milingoti ikishapandwa uvunaji wake unakuwa ni wa ndani ya miaka mitano ambapo mpandaji anaweza kupata faida ya kuvuna nguzo, kama zile ambazo hutumiwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Anasema miti aina ya Mikaratasi kwa kutumia mbegu bora uvunaji wake hutumia miaka 12 tu, tofauti na yule atakayetumia mbegu za kienyeji huchukua muda wa zaidi ya miaka 20 mpaka kuivuna.

Hyera anabainisha kuwa eneo hilo la upandaji ni la serikali na kwamba litabaki kuwa la serikali,lakini miti itakayopandwa itabaki kuwa mali ya wananchi wenyewe walioipanda ambao wataingia mkataba wa maelewano kwa miaka 33 na Halmashauri ya mji wa Mbinga.

Kwa mujibu wa Afisa Misitu huyo,mkataba huo utawawezesha wananchi hao kupanda miti hiyo mpaka kuivuna, ambapo Halmashauri hiyo na serikali kwa ujumla itaweza kupata ushuru wake kupitia mavuno yatakayofanyika kwenye miti hiyo na hatimaye kuweza kuboresha huduma za kijamii.

Baada ya miaka michache ijayo tunatarajia maisha ya wakazi wa Mkoa wa Ruvuma yatabadiilika kabisa kutokana na kufanya mradi wa kupanda miti kibiashara

**Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili,mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917.**